

# **Kuwa Na Nia Ya Kufanya Kazi**

## **(Having a Mind to Work)**

**Na**

**Ellis P. Forsman**

# **Kuwa Nia Ya Kufanya Kazi**

**Na**

**Ellis P. Forsman**

**Octoba 12, 2011**

# Kuwa Nia Ya Kufanya Kazi

## Nehemia 4:6

Neh.4:6, *“Basi tukaujenga ukuta nao ukuta wote ukaungamanishwa kiasi cha nusu ya kimo chake; maana watu walikuwa na nia ya kufanya kazi.”*

### **Kuhusu kifungu:**

Chini ya uongozi wa Ezra na Nehemia, Wayahudi walirudi Yerusalemu baada ya utumwa wa Babeli. Ilikuwa hapo ndipo walipoanza kujenga kuta za Yerusalemu.

Wasamaria walipinga kazi ya kujenga ukuta.

Wayahudi walikuwa na nia ya kufanya kazi; dhahaka, mateso hazikuwazuia.

### **Kuhusu kipeperushi hiki.**

Tunapofikiria kazi, mara nyingi tunafikiri shughuli zetu.

Kimsingi kazi siyo kitu ambacho mtu anaweza kukifurahia kuifanya. Wengine hufurahi, wengine hawafurahi. Kuna sababu. Kazi ni adhabu ya mwanadamu kwa dhambi ya Adamu.

Mwa. 3:17-19, *“Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza nikisema usilaye, ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.”*

Hataiavyo, tunatambua kwamba ni lazima ifanywe na hivyo tunaifanya.

Lakini kwa ulinganifu wa “kimwili” kazi tunayofanya, Mungu ana kazi ya kiroho kwa watu wake. Tunafanya kazi hii kwa sababu ya upendo wetu kwa Mungu na ufalme wake.

Mhu. 9:10, *“Lo lote mkono wako utakalolipata kulifanya ulifanye kwa nguvu zako; kwa kuwa hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima, huko kuzimu uendako wewe.”*

“Nia ya kufanya kazi” ni ile inayo:

## **Hitaji la kufanya kazi**

Mara zote kuna hitaji la kufanya kazi.

Bwana ametupatia kazi yake.

Mat. 28:18-20, *“Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enenderi mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.”*

Tuna wajibu wa kufanya kazi ulimwenguni kote vilevile na nyumbani. Mataifa yote kujumuisha taifa letu!

Kanisa hapa litakuwepo, na litaendelea, tukifanya kazi ya Mungu.

Sote tunapaswa kuwa makini kuvutiwa na kazi.

## **Hamu ya kazi, bila kujali mambo binafsi**

Sote tunamaisha binafsi.

Mara nyingi kuna nafasi yetu binafsi kutoka katika kazi ya Bwana kushiriki kazi zetu na hamu.

Inapokuja kazi ya Bwana, tunapaswa kuachana na tabia hizi.

Lazima tuweke mambo ya Mungu kwanza katika maisha yetu. Mat. 6:33, *“Watu wakawaona wakienda zao na wengi wakatambua wakaendaa huko mbio kwa miguu toka miji yote, wakatangulia kufika.”*

Tunapaswa kujitoa dhabihu katika maisha yetu binafsi. Mfano:

- Yesu
- Paulo. Fil. 2:5, *“Muwe na nia hii ndani yenu, ambayo pia ilikuwa ndani ya Kristo Yesu.”*

Tutatoa dhabihu nini?

Ni jambo kuu kutoa muda wetu sadaka, na matakwa binafsi. Tunapaswa kutoa sadaka na kufanya muda wetu kwa ajili ya mambo ya kiroho.

## **Tutafanya kazi gata katika hali ya kuchukiwa**

Chuki hutafsiri tabia

Tunawajibu vipi wenye chuki?

- Kanisa la kwanza. Mdo. 8:4, *“Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihumbiri neno.”*
- Paulo. 2 Kor. 2:14-16, *“Ila mungu na ashukuriwe aliyetushangiliza daima katika Kristo, naa kudhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu. Kwa maana sisi tu manukato ya Kristo, mbele za Mungu katika wao wanaokolewa, na katika wao wanaopotea; katika hao wa pili harufu ya mauti iletayo mauti; katika hao wa kwanza harufu ya uzima iletayo uzima. Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?”*

Hatuwezi kuruhusu wenye dhahaka watuzuie.

Hatuwezi kukubali kuacha kufanya kazi eti kwa sababu hatuoni matokeo yanayoonekana.

Zingatia Nuhu (miaka 100 kwa majibu madogo au hakuna kabisa). Kazi ya Mungu lazima iendelee bila kujali matokeo yanayoonekana.





